

Algorithmu na Namba Tasa

Namba tasa ni namba kamili ambayo ni kubwa kuliko 1 — kama vile 2, 3, 5, 7, au 11 — inayoweza kugawanyika kwa 1 au yenyewe tu. Lengo lako katika zoezi hili ni kutambua namba tasa zote hadi kufikia 100. Andika hatua ulizotumia kukamilisha kazi hii kabla ya "Lengo," na vilevile ingizo lako na matokeo!

Tafadhali kumbuka kwamba hatua hizo huwataka washiriki wazungushe duara kwenye namba tasa na kukata namba ambazo si tasa. Ili kuhakikisha kwamba nakala hii ya mkufunzi inasomeka, namba tasa ziko kwenye maandishi mekundu na namba ambazo si tasa ziko kwenye maandishi ya kijivu.

1	2	3	4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17	18	19	20
21	22	23	24	25	26	27	28	29	30
31	32	33	34	35	36	37	38	39	40
41	42	43	44	45	46	47	48	49	50
51	52	53	54	55	56	57	58	59	60
61	62	63	64	65	66	67	68	69	70
71	72	73	74	75	76	77	78	79	80
81	82	83	84	85	86	87	88	89	90
91	92	93	94	95	96	97	98	99	100

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Meta na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.

Algorithmu na Namba Tasa



Lengo: Tambua namba tasa zote hadi kufikia 100.



Hatua:

- Andika namba kamili zote kuanzia 1 hadi 100 katika mpangilio wa 10 kwa 10 kwa utaratibu unaoongezeka.
- Kata 1 kisha ukate namba zote ambazo ni vigawe vya 2, isipokuwa 2 (mfano, 4, 6, 8, na kadhalika). Kisha, zungusha duara kwenye 2.
- Chukua namba inayofuata iliyo ndogo zaidi ambayo haijzungushwa duara — katika hali hii ni 3. Kata 1 kisha ukate namba zote ambazo ni vigawe vya 3, isipokuwa 3 (mfano, 6, 9, 12, na kadhalika).
- Endelea vivyo hivyo hadi zibaki tu namba ambazo zimezungushwa duara. Namba hizi ni namba tasa zote hadi kufikia 100.



Ingizo: 100



Matokeo: 2, 3, 5, 7, 11, 13, 17, 19, 23, 29, 31, 37, 41, 43, 47, 53, 59, 61, 67, 71, 73, 79, 83, 89, 97



Algorithmu hii inajulikana kama Kichujio cha Eratosthenes.

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Meta na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.